**TAARIFA YA MAENDELEO YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI**

**TAREHE:** Desemba 03 2020

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)[1] ni Mradi unaoendeshwa na sekta binafsi na kumilikiwa na kampuni inayojitegemea ya Bomba la Mafuta itakayoanzishwa na kuingia makubaliano na serikali hodhi[2] (Uganda na Tanzania). Serikali zote mbili zinatakiwa kukamilisha makubaliano ya nchi hodhi ili kuweza kutekeleza Makubaliano kati ya Serikali Mbili (Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda) kwa ajili ya mfumo wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki yaliyosainiwa tarehe 25 Mei 2017.

Wanahisa wa Kampuni ya Bomba la Mafuta wanatarajiwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Uganda, kupitia Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (TPDC), likiwakilisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kampuni mbili za Kimataifa za Mafuta katika mkondo wa juu: TOTAL na CNOOC.

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ndiyo itakayomiliki miundombinu ya bomba la Mafuta[3] na kutoa huduma ya usafirishaji Mafuta; kampuni hii haitomililki Mafuta yatakayosafirishwa kupitia miundombinu yake. Kampuni ya Bomba la Mafuta itakuwa na jukumu la kujenga bomba, kuliendesha, na kuhakikisha usalama wa muda mrefu na uhakika wa uwepo wa huduma za bomba.

Tathmini za Athari katika Mazingira na Jamii (ESIA) zilifanyika nchini Uganda na Tanzania Ili kuweza kuandaa mipango madhubuti ya kupunguza madhara kulingana na matakwa ya kisheria katika nchi zote mbili pamoja na Viwango vya Kimataifa vya Uwezeshaji Kifedha. Ripoti za ESIA zinatakiwa kuwa wazi kwa

[1] Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ni muundombinu wa kusafirisha Mafuta ghafi wenye urefu wa kilomita 1,443 utakaotokea Kabaale-Hoima nchini Uganda mpaka Chongoleani Peninsula-Tanga nchini Tanzania. Muundo mbinu huu unajumuisha Bomba la inchi 24 linalotunza joto, litalofukiwa ardhini vituo sita vya kusukuma Mafuta (viwili viko nchini Uganda na vinne viko Tanzania), vituo viwili vya kupunguza kasi ya mafuta vyote viko nchini Tanzania pamoja na Kituo kwa ajili ya upakiaji Mafuta melini wa mafuta kilicho katika eneo la bahari Tanga, Tanzania. Mafuta ya Uganda yana asili ya uzito na hali ya nta hivyo kuhitaji mafuta hayo kusafirishwa katika kiwango cha nyuzi joto 50 ili yaweze kufikia kiwango cha kutiririka. Ilikuhakikisha bomba linakuwa na kiwango cha joto kinachohitajika, bomba litapashwa joto kwa njia ya umeme, na kulifanya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kuwa bomba refu zaidi duniani linalopashwa joto kwa njia ya umeme.

2 Makubaliano ya Awali na nchi Hodhi (HGA) yamefikiwa kati ya Mradi na Serikali ya Uganda Septemba 11 2020 na Serikali ya Tanzania Octoba 26 2020. .

[3] Bomba la Mafuta hutoa mfumo bora na salama kwa usafirishaji wa muda mrefu wa Mafuta. Vilevile, vigezo vya usanifu wa mfumo wa bomba vinatokana na viwango vya juu vya kimataifa. Mfumo wa bomba lililofukiwa ardhini ni bora zaidi na ni njia inayotegemewa zaidi katika kusafirisha Mafuta huku ikipunguza madhara katika Mazingira na Jamii (E&S) katika kipindi cha usafirishaji.

umma[4] na wadau wengine kulingana na miongozo ya nchi husika na kuidhinishwa[5] na serikali husika kupitia Mamlaka za Serikali husika na kuwekwa katika tovuti ya Mradi.

Tathmini za mradi wa EACOP za Athari katika Mazingira na Jamii (ESIA) zimetafiti maeneo yote yaliyo chini ya usimamizi maalum na yale yenye umuhimu wa bayoanuai pamoja na vihatarishi katika jamii za uendelezaji na kusanifu njia za kupunguza madhara katika madhara yoyote yanayoweza kutokea kwa ajili ya kulinda njia za kujikimu, viumbe hai na makazi yao katika nchi zote mbili pamoja na kurudisha mkuza wa bomba kama ulivyokuwa Awali na kufanikisha kuepuka madhara katika makazi asilia ya viumbehai na kuchangia kuongeza faida kwa viumbehai vilivyo katika hali hatarishi, Utafiti wa Viumbehai vilivyo katika hali hatarishi katika ESIA pamoja na Utafiti wa Athari kwa Haki za Binadamu umefanyika kwa kuzingatia sheria na miongozo ya nchi za Tanzania na Uganda, pamoja na Viwango vya Utekelezaji namba 8 vya Shirika la Kimataifa la Uwezeshaji wa Kifedha (IFC).

Mradi unatafiti na kuangalia namna ya kushiriki kwa kushirikiana na wadau wengine wa uhifadhi katika programu zinaohamasisha kuchangia kuongeza faida katika maeneo ya nchi kavu na baharini kwa lengo la kuhakikisha aina flani ya viumbe hai na makazi yao iko katika hali bora zaidi baada ya utekelezaji wa Mradi pamoja na kuhamasisha urudishwaji wa uwezo wa jamii wa kujikimu na kujipatia kipato.

Maendeleo ya Mradi yatazingatia viwango vya nchi na viwango vya Kimataifa vya Utendaji vya Shirika Uwezeshaji Kifedha la Kimataifa na vilevile kuzingatia dhamira za mazingira za Kampuni ya Total kwa ajili ya utekelezaji endelevu na kuwajibika katika kupunguza utoaji hewa ya ukaa (kipengele 1 na 2) na kuepuka uchafuzi. Hii ni pamoja na kuwa na usimamizi wa kuzuia uchafuzi, mwitikio wa dharura katika uvujaji wa Mafuta na mipango ya usimamizi wa taka katika ngazi zote za ujenzi na usimamizi wa bomba.

Ardhi itahitajika kwa ajili ya kujenga na kuendesha Bomba la Mafuta na miundombinu inayohusika. Mradi unafuata hatua za msingi ili kuweza kutwaa ardhi ikiwemo ushirikishaji wa wadau, uhakiki mali na uthamini, tafiti za kijamii na kiuchumi, upimaji wa vipande vya ardhi nk. Hatua hizi zinafuata sheria na kanuni za Tanzania pamoja na Viwango vya Utendaji vya Shirika la Uwezeshaji Kifedha la Kimataifa. .

Ni madhumuni ya Mradi kufanya malipo ya fidia, kwa niaba ya Serikali kwa kuzingatia muda unaotakiwa kisheria na Viwango vya Uwezeshaji Kifedha vya Kimataifa. Mradi hautotumia ardhi kwa ajili ya ujenzi wa bomba kabla ya kufanya malipo ya fidia kwa waguswa wanaostahili.

Malipo ya fidia yatalipwa kwa upotevu kutokana na kuhamishwa makazi na/au kiuchumi, kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Mthamini Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na viwango vya Utendaji vya Shirika la Uwezeshaji Kifedha la Kimataifa. Tanzania, Ardhi inayohitajika na Mradi itachukuliwa moja kwa moja na Serikali na itakodishwa kwa Mradi wa EACOP.

Mipango ya Uhamishaji Watu na Makazi (RAPs) ya Maeneo ya Awali (PAs), Bomba la Mafuta na Miundombinu ya Juu ya Ardhi (AGIs) kwa mikoa yote nane lilipokatiza bomba la Mafuta imeshakamilishwa, imewasilishwa kwa Serikali ya Tanzania na imeshawekwa wazi kwa umma.[6]

Mradi wa EACOP unadhamiria kuweka taratibu za namna ya kurejesha kipato kwa Watu Wanaoguswa na Mradi (PAPs) ili kuhakikisha viwango vya Maisha vinarejeshwa angalau kufikia kiwango cha Maisha kabla

---

[4] Ripoti ya ESIA Uganda & Ripoti ya ESIA Tanzania.

[5] Cheti cha Ithibati ya Mazingira kwa Ajili ya shughuli za Mradi wa EACOP nchini Tanzania and Uganda kimeshatolewa.

[6] Mipango Kazi ya Uhamishaji Watu na Makazi (Lugha ya Kiingereza) na Muhtasari wa Mipango Kazi ya Uhamishaji Watu na Makazi .

ya Mradi au kuyaboresha zaidi ikiwezekana, Ulipwaji wa fidia kwa Wamiliki wote wa ardhi na watumiaji wanaoishi kwenye mkuza wa bomba utafanyika kwa kuzingatia utu na kulipwa kwa viwango kamili vya uhamishwaji. Ushirikishwaji wa wadau wote unasimamia kanuni za ushiriki, uzingatiaji wa haki za binadamu, ulinzi wa makundi yaliyo katika hali hatarishi, kutokuwa na ubaguzi, uwezeshaji, uwazi na uwajibikaji.

Mradi unawasihi wadau wake wote kuwasilisha malalamiko kupitia Afisa Mahusiano wa Jamii (CRCs) katika maeneo yao husika, namba ya bure[7], ofisi za Mradi na Wakandarasi wa Mradi pamoja na ofisi za serikali za vijiji. Malalamiko haya yanaweza kuwa ni malalamiko ya kimtazamo au yenye Ushahidi, ikiwemo madhara yanayokisiwa,madhara au kutokuridhika kulikotokana na vitendo vya Mradi au Mkandarasi. Mfumo wa utatuzi wa malalamiko ni wa wazi, umewekwa katika nyaraka naumesambazwa kwa wadau.

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi utafungua fursa zilizopo Afrika Mashariki kwa kuvutia wawekezaji kuangalia fursa mbalimbali zilipo katika ukanda. Mradi utapelekea kuongezeka kwa uwekezaji wa moja kwa zaidi ya asilimia sitini nchini Uganda na Tanzania katika kipindi cha ujenzi. Mafanikio ya mradi yatapatikana Kutokana na ushirikiano chanya baina ya wadau wa mradi.

**-MWISHO-**

**Kwa Mahojiano au taarifa zaidi wasiliana na:**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano,
Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki – Tanzania/ Uganda
Mariagoreth Charles / Stella AMONY
**Ofisi:** +255 22 2214100/4102/4103 or +256 (0) 204 916 157
**Simu za Mkononi :** +255 699 000 341 or +256 794 888 157
**Barua Pepe :** mariagoreth.muangirwa@external.total.com copy to stella.amony@external.total.com
**Tovuti :** www.eacop.co.tz or www.eacop.com

[7] Tanzania - 0800 780 068 na kwa Uganda - 0800 216 600